BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA ARDHI NA MAWASILIANO KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA ARDHI, NYUMBA, MAJI NA NISHATI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019

Mheshimiwa Spika,

Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu Allah (S.W), kwa kutujaalia uzima na afya njema tukaweza kukutana tena katika Baraza hili la Tisa, Mkutano wa Kumi kwa ajili ya kuendelea kuwatumikia wananchi wetu. Aidha, kukushukuru na kukupongeza wewe Mheshimiwa Spika na Wasaidizi wako akiwemo Naibu Spika pamoja na Wenyeviti wa Baraza kwa namna mnavyotuongoza katika Baraza hili. Pia, kukushukuru tena kwa kuniruhusu kuweza kusimama mbele ya Baraza hili ili kuweza kuwasilisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii ya Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Spika,

Pamoja na upya wako kwa cheo hiki cha Uspika lakini umeonyesha ukomavu mkubwa katika kulisimamia Baraza na kuimarisha nidhamu kwa Wajumbe ndio maana hadi sasa chombo chako hiki kinaendelea kuheshimika na wananchi wote wa Zanzibar, Tanzania na Duniani kwa ujumla, tunakuombea kila la kheri na maisha marefu katika majukumu yako haya ya kulitumikia Taifa hili.

Mheshimiwa Spika,

Pia, napenda kutoa shukrani zangu kwa Waziri na Naibu Waziri wa Wizara ya Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati pamoja na Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Wakurugenzi na watendaji wote wa Wizara hii kwa ushirikiano mkubwa waliotoa katika kufanikisha kumalizika kwa kazi hii ya Kamati.

Mheshimiwa Spika,

Vilevile, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Wajumbe wa Kamati ya Ardhi na Mawasiliano kwa mashirikiano waliyonipa katika kipindi chote cha kazi za Kamati na hatimae kufanikisha kazi zetu kwa lengo la kuisimamia na kuishauri Serikali. Baada ya maelezo hayo naomba niwatambue wajumbe wa Kamati hii ambao ni:

1. Mhe. Hamza Hassan Juma - Mwenyekiti
2. Mhe. Suleiman Sarhan Said - Makamu Mwenyekiti
3. Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil - Mjumbe
4. Mhe. Khadija Omar Kibano - Mjumbe
5. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Mjumbe
6. Mhe. Mohamedraza Hassanali - Mjumbe
7. Mhe. Nassor Salim Ali - Mjumbe
8. Mhe. Said Omar Said - Mjumbe

Mheshimiwa Spika,

Aidha, Kamati yetu inafanyakazi na makatibu wawili ambao kwa kiasi kikubwa wamekuwa wakitusaidia sana katika kutekeleza majukumu yetu, makatibu hao ni:

1. Ndg. Fatma Omar Ali - Katibu
2. Ndg. Mwanaisha Mohammed Kheir - Katibu

Mheshimiwa Spika,

Kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Baraza la Wawakilishi liliidhinishia Wizara ya Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati Matumizi yenye jumla ya Tshs.10.664 bilioni kwa ajili ya Fungu N01 kwa Matumizi ya kazi za Kawaida. Aidha, Baraza liliidhinishia Wizara ya Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati kutumia jumla ya Tshs.36.943 bilioni kwa ajili ya Matumizi ya kazi za Maendeleo. Vilevile, kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Wizara iliidhinishiwa kukusanya jumla ya Tshs. 10,035 bilioni kama ni mapato yatokanayo na vyanzo mbali mbali vinavyosimamiwa na Wizara hii.

Mheshimiwa Spika,

Katika hotuba ya Bajeti ya Wizara hii ya Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati kwa mwaka huu wa fedha 2018/2019 Wizara hii imepangiwa Tshs. 11.664 bilioni kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida na Tshs. 87.087 bilioni kwa ajili ya kazi za maendeleo. Aidha, inakadiriwa kutumiaTshs. 98.951 bilioni kwaajili ya utekelezaji mzima wa Fungu N01. Aidha, katika utaratibu mpya wa bajeti inayozingatia programu ya 'PBB', Wizara hii imepangiwa kutekeleza Programu Kuu Nne (4) na Programu Ndogo Nane (8) kama zilivyofafanuliwa katika hotuba hiyo ya bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati.

Mheshimiwa Spika,

Baada ya utangulizi huo mfupi, sasa naomba nitekeleze jukumu lililonileta hapa mbele ya Baraza lako tukufu moja kwa moja kwa kuanza uchambuzi wa Programu hizo kama zilivyokwishatangulia kuelezwa na Mhe.Waziri katika kitabu chake cha hotuba aliyoiwasilisha mbele yetu muda mchache uliopita.

PROGRAMU KUU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA YA ARDHI, NYUMBA, MAJI NA NISHATI

Mheshimiwa Spika,

Lengo kuu la Programu hii ni kuimarisha uratibu katika utekelezaji wa kazi za Wizara pamoja na kukuza ufanisi katika utawala wa rasilimali ardhi katika visiwa vyetu vya Unguja na Pemba. Aidha, programu hii inatekelezwa kupitia Idara ya Mipango, Sera na Utafiti, Idara ya Utumishi na Uendeshaji na Afisi Kuu Pemba.

Mheshimiwa Spika,

Kupitia utekelezaji wa programu ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Wizara, Kamati inaiomba Wizara kwa kushirikiana na Taasisi husika kufanya kazi kwa mashirikiano baina ya Wizara na Washirika wa Maendeleo katika Miradi yote inayokusudiwa kutekelezwa na Serikali kwa kushirikiana na Wafadhili hao wa Maendeleo hapa Zanzibar kuisimamia kwa mujibu wa Sheria zinavyoelekeza.

PROGRAMU KUU YA USIMAMIZI NA UPANGAJI WA MATUMIZI YA ARDHI

Mheshimiwa Spika,

Programu hii inatekelezwa kupitia programu ndogo tatu programu ndogo ya utawala wa ardhi, programu ndogo ya utatuzi wa migogoro ya ardhi pamoja na programu ndogo ya uthamini wa rasilimali.

PROGRAMU NDOGO YA UTAWALA WA ARDHI

Mheshimiwa Spika,

Programu ndogo hii ina jukumu la kuhakikisha usalama wa umiliki wa ardhi kwa wananchi wanaoishi maeneo ya Zanzibar, Ugawaji wa Usimamizi wa Ardhi, Usajili wa Ardhi, Upimaji wa Ramani za Ardhi pamoja na Upangaji wa Miji na Matumizi ya Ardhi yaliyo bora na salama.

Mheshimiwa Spika,

Sambamba na hilo, Kamati kupitia utekelezaji wa programu ndogo hii inaishauri Wizara kupitia Kamisheni ya Ardhi kuandaa mpango mpya wa upitiaji na ugawaji wa maeneo ya eka tatu ambayo yaliotolewa kwa dhumuni la kilimo ambapo hivi sasa wananchi wamebadili matumizi yake na badala yake kujenga nyumba za makaazi

katika maeneo hayo kinyume na taratibu zilizopo kisheria na kukosa sifa za kuwa makaazi bora kwa maisha ya mwanaadamu.

Mheshimiwa Spika,

Kamati yangu inaitaka Serikali kupitia idara hii, kuzipitia upya eka tatu tatu na kuzisimamia zile ambazo kwa sasa bado zina sifa za kuitwa eka tatu kwa ajili ya kilimo kwa ziekewe uangalizi maalum na kuzisimamia ziendelee kuwa ni maeneo ya kilimo, na kuzibadilishia matumizi zile ambazo kwa sasa zimeshakosa sifa za kuitwa eka tatu tatu kwa kuzingatia baadhi yake zimeshajengwa nyumba nyingi za makaazi ya watu na kukosa sifa za kuwa maeneo ya kilimo ili wahusika wapimiwe kisheria na na kupewa hati kwa ajili ya makaazi yao ya kudumu.

Mheshimiwa Spika,

Pia, Kamati yangu imegundua kuwa idara hii ina upungufu mkubwa wa wafanyakazi wataalamu, uhaba wa usafiri na vitendea kazi ikiwemo vifaa vya kisasa vya upimaji jambo ambalo linapunguza kasi ya utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku na hatimae hupelekea kuchelewa kuyapanga na kuyapima maeneo ya miji yetu na vijiji ambapo hupelekea ujenzi holela unaokosesha haiba ya miji yetu kuongezeka.

Mheshimiwa Spika,

Vile vile, Kamati yangu inaiomba Serikali kwa kushirikiana na Wizara husika kuajiri wataalamu wa kutosha katika idara hii ya upangaji miji na matumizi ya ardhi ili kuondokana na changamoto ya ujenzi usiofuata utaratibu na usio na tija kwa taifa letu la sasa na baadae. Pia, Kamati yangu imegundua maslahi ya watumishi wa idara hii ni madogo hasa kwa kuzingatia taaluma yao kuwa ni nyeti na wataalamu wa aina hii ni wachache ambao kwenye makampuni binafsi hulipwa mafao makubwa sana kutokana na utaalamu wao, kwa hivyo Kamati yangu inaiomba Serikali kuangalia upya maslahi ya wafanyakazi wetu hawa ili wafanye kazi zao kwa ufanisi na utulivu mkubwa.

Mheshimiwa Spika,

Sambamba na hilo, Kamati yangu inapongeza jitihada za Serikali za kuwapatia wananchi makaazi bora na ya kisasa, kupitia mradi wa mji mpya wa Ng'ambo maarufu "Ng'ambo Tuitakayo", mradi huu ambao sio muda mrefu utaanza kutekelezwa kuanzia Mtaa wa Kwahani. Hivyo, Kamati yangu inaiomba Serikali kuhakikisha nyumba zitakazojengwa ziwe zinalingana na mazingira ya wanzibari kwani utamaduni wetu huwa tunazaa watoto wengi hivyo katika ujenzi wa nyumba hizo kusiwe na nyumba za vyumba viwili kama ilivyo katika nchi nyengine.

Mheshimiwa Spika,

Vilevile, Kamati yangu inaishauri Serikali pamoja na Wizara husika ujenzi wa mradi huo ungeligawa "block" la mjini kwa mzunguko wa Barabara ya Mtoni, Kwamtipura, Amani, Magomeni, Mpendae, Kiembesamaki, Kikwajuni, Kwahani na Chumbuni, kuliko kuanza kati kati ya mji hapo Kwahani.

Mheshimiwa Spika,
Kamati yangu inaipongeza Kamisheni ya Ardhi kwa kazi kubwa wanazotekeleza kwa umakini mkubwa kwani wamekuwa ni wasimamizi wakubwa katika kusimamia matumizi bora ya ardhi kwa kufuata maelekezo ya Kamati hii kwa asilimia kubwa ambapo imesaidia sana katika kupunguza migogoro ya ardhi.

Mheshimiwa Spika,
Pamoja na hayo, Kamati yangu inaiomba Kamisheni ya Ardhi kuufuatilia mgogoro unaofukuta baina ya wananchi wa Matemwe na Muwekezaji wa Pololo. Kutokana na kadhia hiyo, Kamati yangu imepata mshtuko kwa kuona barua ya Muwekezaji kusimamisha kuendelea kwa mradi mkubwa ambao utasaidia kuongeza pato letu la taifa.

Mheshimiwa Spika,
Hivyo, Kamati yangu inamuomba Mhe.Waziri aufuatilie kwa kina mgogoro na baadae kuhakikisha haki inatendeka kwa Muwekezaji ili aweze kuendelea na mradi huo na kwa upande wa wananchi wote waliopo katika maeneo hayo waangaliwe kwa jicho la kufidiwa sehemu nyengine ambayo wataweza kuendeleza nao mradi wao. Pia, Kamati yangu inaamini Kamisheni ya Ardhi kupitia Waziri wataweza kuuzingatia ushauri wetu wa Kamati kwa maslahi mapana ya taifa hili.

Mheshimiwa Spika,
Kamati yangu pia inaiomba Kamisheni ya Ardhi kuwapatia hati yao ya umiliki wa Ardhi wazee wa eneo la Makangale (Pemba) ambapo Kamisheni hii tayari imeshalipima eneo hilo na kutofautisha mipaka ya eneno la msitu wa Ngezi, kwani kama inavyoelezea Sera ya Ardhi kuwa ardhi yote ya Zanzibar ipimwe na wananchi waweze kuziendeleza ardhi zao bila ya hofu ya kuvamiwa, kunyang'anywa au kuporwa.

Mheshimiwa Spika,

Kamati yangu tena inaipongeza Serikali kwa mradi ulioanza wa kuupima na kuchukua Ramani ya nchi yetu kwa kutumia "Drom" ambapo Chuo Kikuu cha SUZA ndio kimepewa kazi hiyo tunawapongeza kwa kuweza kuwatumia wataalamu wetu wa ndani ambapo tunazidi kuwaongezea ujuzi na kujiamini kiasi cha kutosha, isipokua tu

Kamati yetu inaiomba Serikali wakati wa kupiga picha hizo wazingatie mipaka ya Zanzibar kabla ya Muungano ambapo kilichomo ndani ya mipaka hiyo ndio rasilimali zetu wazanzibari ikiwemo kisiwa cha "Latham Island" au kwa lunga nyengine "Fungu Mbaraka", ambapo inasemekana kuna rasilimali ya Mafuta na Gesi katika eneo hilo, Kwani Ramani hizo ndio zitakazotumika kufanya tafiti mbali mbali kwa Mipango ya Matumizi ya Ardhi kwa sasa na hapo baadae.

PROGRAMU NDOGO YA UTATUZI WA MIGOGORO YA ARDHI

Mheshimiwa Spika,

Malengo makuu yaliyokusudiwa kutekelezwa kwa mwaka wa fedha 2018/2019 ni kuongeza ufanisi katika utoaji wa maamuzi ya kesi zinazohusiana na migogoro ya ardhi, kufanya mategenenzo ya jengo la Mahakama ya Mkoa wa Kaskazini Unguja (Gamba) ili kusaidia huduma hiyo kupatikana kwa urahisi na kwa wakati pamoja na kutoa elimu kwa jamii kuhusiana na upatikanaji wa haki kupitia Mahakama hizo.

Mheshimiwa Spika,

Kupitia programu ndogo hii tena, Kamati inaipongeza Serikali kupitia Wizara hii, kwa kuweka bajeti ya kulikarabati jengo la Mahakama ya Ardhi katika Mkoa wa Kaskazini Unguja kwani tunategemea kukamilika kwa jengo hilo litasaidia kuweza kuwaondoshea wananchi wa maeneo hayo usumbufu wa kuifuata huduma hiyo ya kimahakama katika Mahakama ya Majestik iliyoko Mjini jambo linalopelekea usumbufu mkubwa kwa wananchi ambao wanafuatilia haki zao.
Sambamba na hilo, Kamati inaitaka Kamisheni ya Utumishi Serikalini kuharakisha upatikanaji wa watumishi katika Mahakama ya Ardhi kwani uhaba mkubwa wa wafanyakazi hukwamisha utendaji wa kazi wa Mahakama hizo na kuchelewesha utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi (CCM) kuhusiana na kumaliza migogoro ya ardhi hapa Zanzibar.

Vilevile, Kamati inaitaka Wizara pamoja na Afisi ya Msajili wa Ardhi na Afisi ya Mtambuzi wa Ardhi kukaa kwa pamoja kuandaa mafunzo juu ya umuhimu wa utambuzi na usajili wa ardhi kwa wananchi wa mjini na vijini katika visiwa vyetu vya Unguja na Pemba ili kupunguza idadi ya migogoro ya ardhi inayozidi kuibuka siku hadi siku.

Mheshimiwa Spika,

Pamoja na hayo, Kamati yangu bado inaikumbusha Serikali kupitia Idara ya Utawala na Utumishi kuzingatia watumishi ambao wamepewa nafasi za kushika madaraka ya kuwasimamia wenzao basi ni vyema wakalipwa stahiki zao hasa kwa kuzingatia

majukumu walionayo kuwasimamia wenzao lakini pia wamepata uteuzi huu na Mhe. Rais, mfano halisi wa hilo ni Mwenyekiti wa Mahakama ya Ardhi.

PROGRAMU KUU YA UHIFADHI NA UIMARISHAJI WA MAKAAZI

Mheshimiwa Spika,

Pamoja na majukumu yaliyopangwa kutekelezwa chini ya programu kuu hii, Kamati inaliomba Shirika la Nyumba kwa kushirikiana na Bodi ya Kodi za Nyumba kuandaa mpango mkakati wa kukusanya kodi kupitia nyumba zote za Serikali zinazosimamiwa na Shirika hili.

Mheshimiwa Spika,

Pia, Kamati yangu inalipongeza Shirika la Nyumba hasa kwa upande wa Pemba kwa kuanza kuvifanyia ukarabati mkubwa Nyumba za Maendeleo hapo Madungu (ChakeChake) tunaomba zoezi hili liendelee na kwa hapa Unguja hasa kuzihami Nyumba zetu za Maendeleo. Aidha, Kamati inawataka pia wakaazi wa Nyumba za Maendeleo kuunda Kamati zao ili kushirikiana na Shirika katika kuhakikisha kodi zinalipwa na pia Shirika kuendeleza ukarabati wa Nyumba zote Unguja na Pemba, kwani Shirika kwa kuwatumia wafanyakazi wake huokoa fedha nyingi kuliko zingelipewa Kampuni Binafsi.

Mheshimiwa Spika,

Kutokana na hali hiyo, Kamati yangu bado inaendelea kulisisitiza Shirika letu la Nyumba kuweza kutumia rasilimali zake za Majengo walionayo kukaa na taasisi za Fedha kujenga Nyumba za Makaazi na Biashara ili kuweza kujenga Nyumba na pia kuingia mikataba na mashirika au Makampuni yanayofanya biashara ya kujenga na kukopesha Nyumba **(REAL EASTATES)** ili kuweza nasi kuwa na Miradi Mikubwa itakayoleta tija kwa Shirika pamoja na kuboresha miji yetu ya Unguja na Pemba, kwani kuna watumishi wengi wa Serikali pia sekta binafsi wana mahitaji makubwa ya Nyumba za Makaazi na Biashara.

Mheshimiwa Spika,

Kamati yangu inashangaa kuona hivi sasa kuna mpango wa kujenga nyumba za makaazi kwa mradi wa Ng'ambo tuitakayo lakini mradi huo hauhusishi Shirika la Nyumba ambapo Shirika hilo ndilo lenye jukumu la kusimamia nyumba zote za Serikali, nadhani ni vyema katika mpango huo, Shirika la Nyumba likashirikishwa kikamilifu kwani hata ukusanyaji wa malipo ya nyumba hizo utakuwa katika

usimamizi wa Shirika. Kwani kufanya hivyo kutaondoa mkanganyiko wa juu ya mmiliki halali na msimamizi halali nyumba hizo.

Mheshimiwa Spika,

Licha ya hayo, Kamati yangu inaipongeza Wakala wa Majengo kwa kuanza kazi ya kuwasimamia wakandarasi wote kwenye miradi mikubwa ya Serikali na Binafsi ili kupata Majengo na Nyumba bora zenye kiwango, ingawa Wakala wa Majengo inakabiliwa na changamoto nyingi ikiwemo miradi mikubwa kutokuwa tayari kukaguliwa na wataalamu wa Wakala wa Majengo hasa wanaotoka nje ya Nchi.

Mheshimiwa Spika,

Kwa hivyo, Kamati yangu inawaomba watendaji wote wa Serikali na watu binafsi wanapokuwa na Miradi ya ujenzi jambo la mwanzo kuwaalika Wakala ili kupata ushauri wa utaalamu, kwani hivi sasa tumeshuhudia miradi mingi mikubwa imekuwa inakabiliwa na changamoto ya majengo kutokuwa na kiwango na wakati mwengine mapaa ya baadhi ya majengo hayo kuvuja kama mfereji na mengine hufanya nyufa wakati majengo bado ni mapya hii ni kutokana na kukosa ushauri wa kitaalamu tangu awali. Hivyo, kwa kumtumia Wakala wa Majengo ya Serikali itaokoa fedha nyingi za walipakodi wa Zanzibar pamoja na Serikali kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika,

Kwa muktadha huo, Kamati yangu inaitaka Wakala wa Majengo kujitahidi katika kuwapatia mafunzo wataalamu wake kwani kila siku zikienda majengo makubwa ya kisasa yanajengwa hapa Zanzibar, kwa hiyo ni vyema tukaandaa wataalamu wa kutosha ili kukabiliana na changamoto za majengo ya kisasa.

Mheshimiwa Spika,

Kamati yangu pia inaitaka Wakala wa Majengo kuwaongezea maslahi wataalamu wake wa ndani kwani malipo wanayolipwa hivi sasa ni madogo ambapo wanapofanya kazi katika taasisi binafsi hulipwa mara nne zaidi ya kile ambacho wanalipwa na Wakala wa Majengo jambo hili linaweza kuwashawishi kupitisha michoro isiyokuwa na viwango kwa kushawishiwa na wenye makampuni ya ujenzi. Hivyo, Kamati yangu inarejea kulizungumzia tena suala la maslahi ya wataalamu wa Wakala wa Majengo kwani kazi wanayoifanya ni kubwa mno ya kuokoa fedha za umma kwa hivyo ni vyema maslahi yao kuboreshwa, ili kuwapa moyo wa kuchapa kazi zaidi.

Mheshimiwa Spika,

Vilevile, Kamati yangu inaishauri Wakala wa Majengo wa Serikali kutoa elimu kwa Ofisi zote za Serikali juu ya umuhimu wa uwekaji miundombinu rafiki kwa watu wenye ulemavu katika majengo yetu ya Serikali ili wananchi hao wanapohitaji huduma waweze kupata kwa urahisi na bila ya kikwazo chochote kama watu wengine.

Mheshimiwa Spika,

Kupitia programu ndogo hii, Kamati yangu inaipongeza Mamlaka ya Mji Mkongwe kwa kusimamia kazi zao vizuri ya kuutunza na kuuhifadhi Mji Mkongwe kwani bila ya wao majengo yote ya Mji Mkongwe tusingeliyakuta lakini kuwepo kwao nchi yetu imeendelea kuwa ni kivutio cha watalii kwa kuja kujionea historia kubwa ya Zanzibar kabla ya Mapinduzi ya Zanzibar. Pamoja na lawama na changamoto zilizopo bado elimu kwa wananchi ya kuuhifadhi Mji wetu huu adimu katika karne hizi za sasa.

Mheshimiwa Spika,

Tumejifunza mengi katika kuhifadhi historia za miji Duniani kama ilivyo nchini ya Misri, Saudia Arabia, Uingereza hata Ujerumani, jinsi wanavyohifadhi historia ya majengo ya nchi zao ambapo kuna Majengo tangu kabla ya kuingia Uislamu hadi leo kuna Majengo hayo yamehifadhiwa ikiwa ni sehemu ya historia na kusababisha kuingia watalii wengi na kuongeza pato la Taifa. Kwa hivyo, ni vyema na sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar tukawapa kila msaada unaohitajika Mamlaka hii ili waweze kutekeleza majukumu yao vizuri.

Mheshimiwa Spika,

Vilevile, Kamati yangu inapongeza jitihada zinazochukuliwa na Mamlaka hii kupitia Ubalozi wa Oman nchini kwa kutia saini mkataba wa Ukarabati mkubwa wa Jengo la Bait - El - Ajab jengo lililobeba na kusheheni historia ya Zanzibar. Aidha, Kamati yangu inaitaka Mamlaka kusimamia kwa karibu ukarabati wa jengo hilo kwani kwa muda mrefu sasa tumekuwa tunakosa fedha za kigeni kwa kutokutumika kwa jengo hilo la kihistoria.

Mheshimiwa Spika,

Pia, Kamati yangu inaiomba Wizara hii kwa kushirikiana na Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji Mji Mkongwe kuharakisha kuifanyia mapitio na marekebisho Sheria nambari 4 ya 2010 ili kwenda na wakati.

PROGRAMU KUU YA USIMAMIZI WA HUDUMA ZA MAJI NA NISHATI

Mheshimiwa Spika,

Programu hii inatekelezwa kupitia Mamlaka ya Maji (ZAWA), Mamlaka ya Udhibiti wa Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia (ZPRA), Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati (ZURA), Shirika la Umeme pamoja Idara ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika,

Kupitia Programu Kuu hii, Kamati inaiomba Serikali kwa kushirikiana na Wizara kuharakisha uundwaji wa Kampuni ya Mafuta ya Serikali pamoja na Bodi ili kuipa nguvu Mamlaka ya Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia kuweza kufanya kazi zake kwa ufanisi na umahiri.

Mheshimiwa Spika,

Kamati yangu imegundua kupitia programu kuu hii bado tatizo la upatikanaji wa maji safi na salama hapa Zanzibar bado limekuwa ni changamoto kubwa hasa katika maeneo ya Mkoa wa Mjini Magharibi, hapa Zanzibar, tumeona jitihada nyingi zikichukuliwa na Serikali kupitia miradi mbali mbali inayosimamiwa na ZAWA lakini bado tatizo la upatikanaji wa maji safi na salama limekuwa na mtihani mkubwa.

Mheshimiwa Spika,

Kamati imegundua changamoto nyingi ikiwemo kukauka kwa baadhi ya vianzio vya maji kumepelekea maji kupungua kwenye vianzio hivyo, pili uvamizi wa vianzio vya maji kwa wananchi kujenga karibu na vianzio vya maji pia limekuwa tatizo sugu, tatu uchakavu wa mabomba ambayo mengi yamekuwa yamejaa “calcium”, na mengine kupasuka ovyo pamoja na baadhi ya wananchi kujenga juu ya mabomba ya maji kusababisha upasukaji wa mabomba hayo na mengine kuziba kabisa.

Mheshimiwa Spika,

Ili kuondoa tatizo hilo, Kamati yangu inaitaka Mamlaka ya Maji (ZAWA) kuharakisha kuviunga visima vilivyochimbwa na Ras - El - Khaimah ambapo tunaamini ikiwa vitaungwa visima hivyo basi kwa zaidi ya asilimia 80 tatizo hilo litaondoka, kwani hatuoni sababu visima hivyo kuwa vimechimbwa kwa gharama kubwa lakini vimechwa bila ya kuungwa wakati huo huo tunaendelea kuchimba vyengine hii inaonyesha kuwa hatukuwa tayari kuchimbiwa visima vile wakati fedha zile ni kodi ya wananchi wao ambapo wameamua kutusaidia sisi.

Sambamba na hilo, Kamati yangu inaitaka Mamlaka ya Maji (ZAWA) kuhakikisha wanakamilisha mchakato wa upatikanaji wea fedha za mradi wa India ili kusaidia kuondoa tatizo la maji hapa Zanzibar ambapo wenzetu Tanzania Bara tayari wameshaanza kufaidika na fedha hizo za mradi wa Serikali ya India. Pia, Kamati yangu inaendelea kuitaka Wizara pamoja na Mamlaka hii kuchukua hatua muafaka za kuanza zoezi la kuondoa majengo yote yaliojengwa katika maeneo ya hifadhi ya vianzio vya maji kwa upande wa Unguja na Pemba.

Mheshimiwa Spika,

Miongoni mwa changamoto kubwa inayoikabili hivi sasa Shirika la Umeme ni kukabiliwa na Deni kubwa la Umeme kutoka ZAWA ambapo linasababishwa na udhaifu mkubwa wa ukusanyaji wa bili za Maji ambapo limekuwa ni tatizo sugu kwani kwanza maji hayapatikani kwa wakati katika maeneo mengi, lakini pia katika maeneo mengi bado ZAWA hawajaweka mita za maji katika majumba na sehemu za biashara ambapo wateja wangeweza kulipia bili hizo kupitia simu za mkononi kama ilivyo kwa mita za TUKUZA.

Mheshimiwa Spika,

Ili kuondokana na tatizo hili, Kamati inaitaka ZAWA kutafuta Kampuni ya kufunga Mita za Maji katika maeneo yote yanaopata maji ili kuweza kuongeza mapato ambayo yataweza kusaidia kulipia bili pamoja na Deni la Umeme na pia kusaidia kuboresha miundombinu ya maji mijini na vijijini bila ya hivyo Mamlaka itaendelea kusuasua kwani inahitaji fedha nyingi katika uendeshaji wa Mamlaka hiyo pamoja na kuwapatia maji safi na salama wananchi. Kwa hivyo, Kamati inaitaka ZAWA kutafuta Kampuni kuingia mkataba wa usambazaji wa Mita hizo ili kuweza kukusanya mapato kama yalioyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika,

Kupitia programu kuu hii, Kamati yangu inapongeza sana Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati (ZURA) kwa kazi kubwa wanayoifanya kwani tangu kuanzishwa kwa Mamlaka hii wananchi wamekuwa wakipata huduma za Maji na Nishati zilizo bora zenye viwango vilivyo imara na endelevu, kwani kwa kipindi kirefu sasa hatujasikia magari kuharibika kutokana na mafuta yaliyochakachuliwa kwasababu ZURA mara kwa mara wamekuwa wakivikagua vituo vya mafuta na Bandarini wakati wa kushusha mafuta, Kamati yangu inaipongeza ZURA kwa kuweza kuleta mpango wa kulihami na kulipangia matumizi eneo la Mangapwani ambapo inategemewa kujengwa Bandari maalum itakayoshughulikia kupakia na kuteremsha Mafuta na Gesi Asilia pamoja na kujenga Bohari kubwa za kuhifadhia mafuta na Gesi

Asilia ambapo tunaweza kusambaza katika nchi nyingine jirani baada ya kumalizika mradi huo.

Mheshimiwa Spika,

Pamoja na hayo, Kamati yangu inaitaka ZURA kushirikiana na Kamisheni ya Ardhi kuhakikisha inatenga maeneo maalum kama fidia kwa wawekezaji wote waliowekeza miundombinu ya kuhifadhia mafuta katika "DEPORT" ya Mtoni katika eneo hilo la Mangapwani ili kuendeleza shughuli zao za kuhifadhia mafuta.

Pia, Kamati yangu inaitaka Serikali kuhakikisha kuwa wawekezaji watakaohamishwa Mtoni kwenda katika eneo la Mangapwani kulipwa fidia inayostahili kwani miongoni mwao wanakabiliwa na madeni makubwa ya Mabenki ambapo walikopa kwa ajili ya uwekezaji huo.

Mheshmiwa Spika,

Kamati yangu inapongeza tena jitihada zinazochukuliwa na ZURA kwa kukamilisha maandalizi ya ujenzi wa jengo lao jipya la kisasa ambalo litaweza kuibeba Wizara nzima. Kutokana na mafanikio hayo, Kamati yangu inapenda kutumia nafasi hii kwa kumpongeza sana Mkurugenzi Mkuu wa ZURA kwa ubunifu na umakini mkubwa katika kazi zake kwa kushirikiana na wasaidizi wake.

Mheshimiwa Spika,

Kamati yangu inatoa pongezi maalum kwa Shirika la Umeme Zanzibar kwa kazi kubwa wanayoifanya kutupatia umeme Mijini na Vijijini, kwa kweli Shirika hili lilikuwa likikabiliwa na changamoto nyingi za madeni na wizi wa uungaji wa umeme pamoja na udokozi ndani ya Shirika lakini kwa hivi sasa tunaipongeza Bodi pamoja na Uongozi na Utawala wa Shirika kuamua kwa makusudi kupambana na vitendo hivyo na hivi sasa Shirika hilo lipo vizuri sana kiutendaji. Aidha, pongezi kubwa zaidi kwa kazi inayoendelea hivi sasa ya kuvipatia umeme vijiji na visiwa vidogo vidogo ambavyo havijawahi kupata umeme tangu asili na jadi jambo ambalo litasaidia kuinua uchumi kwa wananchi wa maeneo hayo pamoja na kupunguza umasikini mkubwa kwa wananchi hao.

Mheshimiwa Spika,

Pamoja na mafanikio hayo, Shirika la Umeme bado linakabiliwa na changamoto ya madeni makubwa wanayodai kutoka katika taasisi mbali mbali za SMZ na SMT pamoja na baadhi ya wananchi. Kutokana na hali hiyo, Kamati yangu inazitaka taasisi hizo kulipa madeni yao kwa haraka kwani huduma za Umeme wanazopatiwa

zinaligharimu kiasi kikubwa cha fedha Shirika hilo. Na wakumbuke kuwa bila ya kupata Umeme huu basi kazi zao zitashindwa kutekelezeka kwani Umeme ni maisha na ndio chachu ya maendeleo katika kila Sekta.

Mheshimiwa Spika,

Vilevile, Kamati yangu inaitaka ZECO kuhakikisha kuwa inatayarisha mpango maalum wa upatikanaji umeme mbadala kwani Zanzibar inategemea kianzio kimoja tu jambo ambalo halina tija nzuri kwa Taifa, kwa hivyo tunawaomba kwa kushirikiana na Idara ya Nishati waanze kutafuta vianzio mbadala vya Umeme kwani ni vyema kuharakisha zoezi hilo ili tuweze kuwa na Umeme wetu wenyewe na wenye uhakika.

Mheshimiwa Spika,

Kamati yangu inapenda kuchukua fursa hii kuipongeza Serikali kwa kuleta Sheria ya Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar ambapo imepelekea kuanzishwa kwa Mamlaka ya Udhibiti wa Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar, ambapo katika hatua za mwanzo tayari imeanza kazi zake, Kamati yangu inaitaka Kamisheni ya Utumishi wa Umma kuipatia wafanyakazi wa kutosha Mamlaka hii. Vile vile, Mamlaka inahitaji wataalamu, hivyo Kamati inaishauri kuendelezwa kitaaluma watendaji wa Mamlaka hiyo, hasa kwa kuzingatia kuwa hapa Zanzibar sekta hii ni ngeni na hatuna wataalamu wa kutosha.

Mheshimiwa Spika,

Kamati yangu inaendelea tena kuishauri Serikali kuharakisha uundaji wa Kampuni ya Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar (ZPRA), Kampuni ambayo ndio itakayokuwa na mamlaka ya kuingia mikataba ya utafiti ya utafutaji na uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia hapa Zanzibar. Pia, tunashukuru kwa hivi sasa harakati za utafiti huo wa mafuta hapa Zanzibar tayari zimeanza lakini hadi sasa Kampuni bado haijaanzisha jambo ambalo huko mbele linaweza kuja kutuletea changamoto hasa katika Mikataba ambapo tumeshuhudia wenzetu Tanzania Bara wamepata mitihani mikubwa katika ufungaji wa Mikataba kwasababu masuala haya yanahitaji wataalamu waliobobea, wenye uzoefu na uaminifu mkubwa na kwa kuzingatia kuwa sekta hii imegubikwa na vitendo vya rushwa duniani hasa katika Mikataba, kwa hiyo tunaiomba Serikali kuzingatia ushauri wetu huo.

Mheshimiwa Spika,

Kamati yangu inaipongeza Idara hii kwa kazi kubwa inayoifanya katika kuhakikisha huduma ya nishati inapatikana hapa Zanzibar kufanya tafiti mbali mbali ambazo zitasaidia kupatikana kwa nishati mbali mbali hapa Zanzibar, kwa sababu bila ya

Nishati hakuna maisha. Kwa muktadha huo, Kamati yangu imepata taaluma kubwa kupitia Idara hii ya Nishati kwa hiyo Kamati yangu inaitaka Idara hii kushirikiana na Shirika la Umeme kutekeleza zile tafiti ambazo zimeshafanyika za kupatikana nishati mbadala ya jua, upepo pamoja na mawimbi ya bahari.

Mheshimiwa Spika,

Vilevile, Kamati yangu inaipongeza Idara hii kuwa ni chimbuko la wataalamu ambao waliandaliwa na hivi sasa kushika nafasi mbali mbali katika Idara na Mamlaka nyengine zilizoanzisha ikiwemo Mamlaka ya Udhibiti na Usimamizi wa Mafuta na Gesi Asilia.

Mheshimiwa Spika,

Kamati yangu inaiomba Idara hii ipatiwe watumishi wengine hasa kwa kuzingatia wengi wao wameazimwa au kuhamishiwa katika taasisi nyengine, Kamati yangu pia inaitakla Wizara kuwapatia jengo linalolingana na mazingira ya taaluma yao pamoja na vitendea kazi hasa "computer" kwani kwa kipindi kirefu wataalamu wetu walikuwa wanatumia "Laptop" zao kufanyia kazi za Idara jambo ambalo linaweza kutoa nje siri za mipango ya Serikali. Lakini pamoja na hayo, tunaipongeza sana kazi kubwa inayofanywa na Idara hii isipokuwa tu ushauri wetu kuwa kuna vijana wengi ambao wamesoma masomo ya sayansi hasa katika fani ya mafuta na Gesi Asilia waweze kuajiriwa ili waje kulitumikia Taifa lao kabla ya kusambaratika na hatimae tukawakosa wataalamu hao.

Mheshimiwa Spika,

Aidha, Kamati yangu baada ya kuzipitia Programu zote nilizozitaja hapo kabla imeona kiwango cha fedha kilichotengwa kwa Idara hii ni kidogo ukilinganisha na ukubwa wa Idara hii ambayo ndiyo muhimili wa Serikali yetu na bado inakabiliwa na changamoto nyingi zinazohitaji kufanyiwa kazi zikiwemo zile za ubovu na uchakavu wa majengo ya Ofisi, uhaba wa vitendea kazi, uhaba wa usafiri kwa ajili ya Idara mbalimbali.

Mheshimiwa Spika,

Mwisho, napenda kukushukuru tena kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha maoni ya Kamati yangu kwa niaba ya Kamati pamoja na kuwashukuru Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwa kunisikiliza, sasa nawaomba Wajumbe wa Baraza lako waijadili na hatimae waiunge mkono bajeti hii ili wamuwezeshe Waziri kufanikisha na kutekeleza yale waliojipangia katika mwaka wa fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Spika,

Kwa niaba yangu na kwa niaba ya Kamati ya Ardhi na Mawasilano naunga mkono hoja hii na naomba kuwasilisha.

Ahsante,

Hamza Hassan Juma
Mwenyekiti,
Kamati ya Ardhi na Mawasiliano,
Baraza la Wawakilishi,
Zanzibar.